# KIKOKOTOO

## DAVID NGOCHO SAMSON

MOGAMBI EMPIRE

**Kimechapwa na;**

Mogambi Studios Sumbawanga.

0629077792/0744509465

**Uhariri**

Joseph Kyando

0754588152

**Usanifu kurasa**

David Ngocho Samson

0629077792/07449465

dvdngocho2@gmail.com

**Usanifu Jalada**

Kindo Arts

0746997969

© David Ngocho Samson, 2021

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kupigisha chapa, kutafsiri kusambaza au kukitumia kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi.


**ISBN 978-9976-5516-2-4**


**Hii ni kazi ya ubunifu, isichukuliwe kuwa ni uhalisi wa mambo. Majina ya watu, makampuni na mashirika yaweza kuwa ya kweli, lakini humu yametumika tu kinadharia. Siyo kwa uhalisi wake. Ni katika kunogesha tu simulizi hii ya kubuni.**


**RIWAYA NYINGINE KUTOKA KWA MWANDISHI DAVID NGOCHO SAMSON**


- **Mheshimiwa The Don**
- **Tineja**
- **Siri Ya Marehemu**
- **Nadhiri Batili**
- **Kazi Ya Mzungu**
- **Mateka Wa Huba**
- **Hamaniko (mkusanyiko wa simulizi fupi fupi)**
- **The Bad Seed- Pamela (Imeandikwa kwa kiingereza)**





- Riwaya -
Tineja
DAVID NGOCHO SAMSON


Riwaya
KIKOKOTOO
David Samson Ngocho


David Ngocho Samson
Riwaya
SIRI YA MAREHEMU


David Samson Ngocho
Nadhiri Batili


DAVID NGOCHO SAMSON
MHESHIMIWA
The Don

# KIKOKOTOO

## 1

## UTANGULIZI

Hakuna aliyejua sababu ya madhila yaliyomkumba mstaafu, tena ambaye enzi za ujana na maisha yake ya Kazi, alikuwa mtu aliyekuwa na nafasi nzuri, na maisha yaliyotosha sifa za kuitwa maisha bora. Lakini fununu mitaani zilienea kuwa, mstaafu huyo, afisa wa serikali, ilisemekana kwamba aliingia mkataba na kampuni moja ya ukopeshaji fedha miaka michache kabla ya kustaafu kwake.

***

Alipozinduka, alikuwa hospitalini, maji ya drip yakitiririka taratibu na

kuingia mwilini mwake kupitia sindano iliyochomwa mkononi mwake. Alijitutumua na kujaribu kunyanyua kichwa chake lakini alihisi uzito usiomithilika sambamba na maumivu makali kiasi cha kuhisi kichwa kinauacha mwili. Nesi aliyekuwa anamhudumia alipomuona mgonjwa wake akihangaika, alimshauri alale na asifanye jambo lolote ambalo lingemzidishia maumivu.

Hakuwa mkaidi, alimsikiliza nesi na kutuliza kichwa chake kwenye godoro huku maumivu yale makali yakimpa wazimu. Maana hakujua kama alipatwa na kizunguzungu au maruweruwe. Kwake yote yalikuwa sawa tu. Alijituliza taratibu, huku

kuwa kwake macho wazi, kukimpa nafasi ya kufunguka fahamu zake.

Taratibu fahamu zake ziilianza kumrejea moja baada ya nyingine. Na kwa kweli, hazikumpa nafuu yoyote aliyotarajia. Maisha yake siku za karibuni yalikuwa hayasomeki kabisa. Alishindwa kujua ni wapi alipokosea kiasi cha kuyapa mwelekeo hovyo kabisa maisha yake, tena wakati ambao alidhani angepata fursa ya kufurahia maisha baada ya kulitumikia taifa kwa uaminifu kabisa.

Kijana wake wa mwisho, kitinda mimba, Mutahaba, au mwite tu Nuts, alikuwa ndani ya gereza kwa tuhuma za ujambazi na mauaji. Kijana mdogo tu wa miaka thelathini kasoro mmoja.

Alikuwa kijana wake wa pekee kwa sasa baada ya kaka zake kusemekana kwamba walikwishatangulia mbele za haki na kwa ugumu wa maisha na ukata aliokuwa nao, hata dhamana ilikuwa imeshindikana kwa ajili ya kumweka huru kijana wake Muta.

Muganyizi hakuwa na mke kwa takribani miongo miwili sasa. Ingawa alimpenda sana mkewe, ajali iliyomuacha na kilema cha mguu, haikumbakizia mke wake kipenzi mama Rutashobya. Alijitahidi na aliamini alikuwa baba na mlezi makini kwa wanawe wanne na hasa yule kitinda mimba, Muta.

Hakutaka kabisa wanae wapitie masahibu aliyopitia yeye enzi za utoto

wake. Alipokumbuka umande na umbali aliotumia kila siku kwenda na kurudi shule bila viatu hata kufikia hatua ya kupasuka miguu, Muganyizi alijibidiisha kwenye kazi wanae wasiyapitie hayo.

Mungu alimjaalia, kwani yeye alisoma enzi za mwalimu, elimu bila malipo, kwa ufadhili wa serikali, na hatimaye kubarikiwa kazi katika wizara ya elimu na kupata cheo cha afisa elimu wilayani Sumbawanga kama ajira yake ya kwanza. Bidii yake ikamwezesha kusomesha wanae shule za kisasa. Shule za malazi nchi jirani ya Kenya. Vijana hao walipofuzu elimu zao za awali, msingi na sekondari, wakapata nafasi ya kusoma

elimu ya juu katika vyuo vikuu mbalimbali.

Familia yake ilikuwa ni mfano wa kuigwa. Kijana wake wa kwanza Rutashobya alifanikiwa kupata shahada yake ya biashara chuo kikuu Cha Dar es salaam na baadaye akaendelea na shahada ya uzamivu chuo Kikuu Cha Oxford nchini Uingereza, na alipotokea hapo na kurejea nyumbani, serikali ikamwajiri kuitumikia katika taasisi nyeti kabisa kwa uchumi wa nchi, Benki kuu ya Tanzania (BOT).

Kijana wa pili, Byarugaba yeye pia alifuzu mafunzo ya uhasibu pale IFM na baadaye akaendea shahada yake ya uzamivu katika chuo Kikuu cha

Witwatersrand nchini Africa ya kusini, na baada ya hapo alirejea nyumbani na kuajiriwa na shirika la umeme TANESCO makao makuu kama mhasibu.

Binti yake wa pekee Kokushubira, yeye aliamua kuwa mwalimu, hivyo mara baada ya kuhitimu shahada yake ya kwanza pale chuo Kikuu Cha Dar es salaam, hakusita kwenda kufundisha huko manispaa ya Morogoro.

Mutahaba alikuwa kijana wake wa mwisho. Kipenzi cha familia. Huyu alizaliwa na kujikuta katika familia iliyosheheni ukwasi na furaha. Kila alichohitaji alikipata bila shida wala

kuwaza. Alijikuta akiishi maisha ya kifalme, asiijue shida wala rangi yake.

Miaka ikasonga, maisha yalizidi kuchanua na kunawiri. Familia ya Muganyizi ilibarikiwa. Lakini nani kaiona kesho?

Ilikuja taarifa, haikuwa nzuri. Rutashobya kijana wake mkubwa, alituhumiwa kwa ubadhirifu na upotevu wa kiasi kikubwa cha fedha za umma katika benki kuu ya taifa (BOT). Hali ikawa tete. Kesi ikatinga mahakamani, ikathibitishwa na mahakama kwamba ni kweli. Haikuwa kweli, hata hivyo, Ruta akaona kuliko jela bora awe mkimbizi ughaibuni. Bila kuacha unyayo Ruta akafutika nchini. Mahakama

ikaamuru mali zake kufilisiwa. Kwa mara ya kwanza familia ya Muganyizi ikapata doa.

Kwa kiasi fulani hali hiyo iliitikisa sana familia ya Muganyizi, kila Kona habari zikawa Ni juu ya familia hiyo, huku raia wakiinyoshea vidole na kuwaita wezi, mafisadi na hata kuwaombea balaa.

Kutokana na hali hiyo, Byarugaba kijana wake wa pili, aliacha kazi na kuamua kufanya biashara binafsi. Fununu zikaeleza kuwa hakuacha Kazi bali naye kama kaka yake alifukuzwa kazi kwa sababu ambazo hazikuwa na mashiko, wengi wakihusisha tukio hilo na ile kashfa

iliyomkumba kaka yake, Rutashobya, ubadhirifu wa fedha za umma.

Baada ya kufanya maamuzi ya kuacha kazi na kuamua kufanya biashara, Mungu hakumtupa mkono Byarugaba, biashara yake ya electronics ilishika kasi, hata akawa Ni msambazaji mkubwa wa vifaa vya electronics jijini Dar es salam. Alikuwa na duka kubwa kabisa katika moja ya mitaa maarufu Kariakoo. Hakuishia kusambaza Dar es salaam pekee. Byarugaba alikuwa na mawakala kila mkoa nchini kwa kipindi cha muda mfupi sana.

Katika harakati zake za kibiashara, safari moja Byarugaba alisafiri kufuata mzigo huko ng'ambo, nchini China.

Haikujulikana nini hasa kilitokea, lakini Byarugaba hakurejea tena nchini. Hali iliyoipa familia yake wasiwasi mkubwa. Wakati, familia ya Muganyizi inaanza kukubaliana na sintofahamu ya kijana wao kupotelea ng'ambo, taarifa zilizothibitishwa na ubalozi nchini China, baadaye zilidai Byarugaba na kaka yake Rutashobya walikamatwa kwa kujihusisha na biashara haramu ya madawa ya kulevya na kuhukumiwa kunyongwa. Habari hizo zilimfika mzee Muganyizi kama mshituko, zilimfadhaisha mno mzee huyoi kiasi cha kumfanya apoteze kabisa ufanisi katika kazi huku afya yake ikiporomoka kila kulipokucha! Kama isingekuwa Muta, Muganyizi ingekuwa habari za jana.

Asingemudu kuukabili msiba huo mkubwa wa vijana wake wawili. Si kwa sababu Muta alimsaidia kuukabili msiba ule bali Muta sasa alibaki tumaini pekee la mzee huyu.

Kutokana na sonona, Muganyizi aliamua kutumia muda wake mwingi kumuomba Mungu na kufanya kila liwezekanalo ili kumsimamisha Muta.

Muta, tofauti na wanawe marehemu, hakuwa na kazi wala hakujua namna ya kujisimamia. Maisha yake yote hata kufikia miaka ishirini na kenda, maisha kwake ilikuwa ni matumizi tu, hakujali namna na wapi zilitoka, pesa zilitumika tu huku zikiingia. Alizoeshwa hivyo.

Vifo vya Ruta na Byarugaba vilikuwa pigo kubwa sana kwake Muganyizi lakini hofu yake kubwa sasa ilikuwa juu ya mwanae ambaye sasa alijutia malezi aliyompa na kujilaumu.

Alifanikiwa kumtafutia kazi, lakini Muta hakutaka kabisa habari za kazi. Hakuzoea kufanya kazi, alichojua ni kufanyiwa kazi. Vipi aanze kumuita mtu mwingine bosi ilhali yeye alikuwa kazoea kuitwa bosi? Ilikuwa changamoto ambayo hakuwa tayari kuikubali. Nyota iliyong'ara sasa ilianza kufifia na kupotea. Muta alipoteza dira. Muganyizi, hofu juu ya mwanae ikamtafuna na kumdhoofisha. Kila alichojaribu kufanya ili kuyapa dira maisha ya

mwanae kilimuonesha ni kwa namna gani alikuwa amechelewa.

Jioni moja, aliamua hana namna nyingine zaidi ya kumhoji Muta anataka nini. Bila kusita, akajibiwa 'pesa', pesa nyingi za kutosha kuanzisha biashara kubwa au kampuni. Muganyizi akajipata njia panda. Pesa hakuwa nayo. Tangu walipopata msiba ule mkubwa, ni kama dunia iliwatenga na kuwapuuza, hata maswahiba wake wa karibu, nao walipotea. Jambo hilo la mtaji kwa Muta likauchoma moyo wake na kumtia sonona zaidi, lakini hakutaka kulipuuza. Alijikuta akilizingatia mno na kuliwazia sana.

Usiku wa siku hiyo hakupata usingizi mapema. Muganyizi alihisi mawazo yake yanamzomea kwa kila mbinu aliyotafakari kutumia kukabili hali ya mwanae. Nyumba yake kubwa sasa ilionekana kujawa na majitu ya kutisha, kila kona ya nyumba ile ilikuwa ni kana kwamba inamzomea. Kichwa chake kilimpwaya kabisa.

Usiku wa saa tisa, Muganyizi alijikuta akijicheka kwa dharau. Umri nao ulikuwa unamtupa mkono, ilikuwa imebaki miaka mitatu kustaafu! Alinyanyuka kitandani akawasha taa kisha akajitazama kwenye kioo kikubwa cha chumbani! Hakuliona lile tabasamu lililozoeleka. Ngozi yake sasa ilikuwa na makunyazi kibao na hata kipara chake kilichong'ara

zamani sasa kilifubaa na kutengeneza taswira ya bonge la kovu.

Wazo hilo la uzee likaamsha wazo jipya. Sasa alirejea kitandani na kupata usingizi. Alipoamka asubuhi alijinyoosha na kujitazama tena kwenye kioo. Alijaribu kutabasamu, kwa mbali akaona nuru. Aliingia bafuni na kuoga huku akiimba wimbo wa Bob Marley, no woman no cry! Alitoka na kuingia kwenye gari lake na kuelekea kazini.

Ilikuwa ajabu kidogo. Siku za hivi karibuni hakuonekana kabisa kutabasamu, lakini leo, ah! leo alijawa na matumaini yaliyompa fursa ya kutoa tabasamu mwanana lililowashangaza watu ofisini. Aliingia

ofisini akiwa mwingi wa furaha. Alikuwa keshafanya maamuzi yangu Jana usiku. Hapa alikuwa amekuja kwa kusudi moja tu la utekelezaji. Aliketi kituoni, akapaisha macho yake dirishani, akatazama nje kwa muda, akawa anayaona magari yakipita barabarani kutokea kwenye ofisi hiyo ambayo ipo kwenye gorofa ya pili katika jengo Hilo la serikali. Alitazama kwa namna ambayo ilionesha huenda ingelikuwa mara ya mwisho kuitumia meza hiyo kwa Kazi zake za kila siku. Uamuzi wake ulikuwa kustaafu kazi. Alipojiridhisha na alichokuwa anakitazama, mzee Muganyizi alirejesha akili yake ofisini hapo. Akavuta keyboard ya komputa yake ya ofisini, akatuliza mawazo na

kuruhusu vidole kudurusu kifaa hicho. Aliandika barua, barua ya kuomba kustaafu mapema. Ulikuwa uamuzi mgumu kufanya, lakini aliamini ulikuwa uamuzi sahihi. Lengo lake likiwa kwamba wakishaprocess taarifa zake, atapokea pensheni yake na hiyo iwe mtaji kwa mwanae Muta kutimiza ndoto yake ya kumiliki biashara aliyokusudia. Alifanya hivyo.

Baada ya kumalizika taratibu zitakiwazo, sasa ilibaki hatua moka ya mwisho. Kupata pesa zake benki, pesa ambazo zingemfaa kijana wake Mutahaba. Huko ndiko alikodondoka na kuzimia na kujikuta hospitalini, akiwa ana drip mkononi.

# 2

Baada ya kutoka hospitalini na kurejea nyumbani, Muganyizi aliendelea kujiuliza nini hasa kilichomtokea. Kesho yake asubuhi alitamka mapema akikusudia kuwahi kwenda katika tawi la kampuni moja ya ukopeshaji fedha, alikopata kukopa fedha miaka michache iliyopita. Lengo la kwenda kule ilikuwa ni kujiridhisha kwamba kuna kosa lilikuwa limefanyika benki ambalo lilipelekea fedha zake za malipo ya kustaafu kupelekwa kwenye kampuni ile kimakosa kama ilivyoonekana kwenye taarifa za akaunti yake ya benki. Bank statement..

Kumbukumbu zake zilikuwa sahihi kabisa. Ilikuwa ni takribani miaka miwili sasa tangu alipokopa fedha kwenye ile kampuni kwa ajili ya kushughulikia kesi ya mwanawe Muta, kipindi hicho Muta alihusishwa na wizi kwa njia ya mtandao, ambapo ilisemekana aliibia kampuni moja ya kusambaza filamu za kibongo kitita cha shilling million tano.

Muganyizi alikopa katika kampuni ile fedha taslimu tsh million tisa kwa makubaliano kwamba miaka michache mbeleni angelipa fedha hiyo kwa riba baada ya kupokea pensheni yake atakapostaafu. Kampuni ilijitanabaisha kuwa na riba ndogo Sana ya asilimia kumi tu.

Ajabu ni kwamba, baada ya kuandika barua ya kuomba kustaafu na kukubaliwa, ilionekana kwamba kiasi cha zaidi ya Tsh million mia moja ambazo alikuwa apokee kama pensheni kilihamishwa kutoka kwenye akaunti yake na kutumwa kwenye akaunti ile ya mikopo kulipa deni alilokopa kutoka kampuni ile. Taarifa hiyo Ilikuwa nzito mno kwake kuipokea na ndio maana alijikuta hospital asijue vipi alifika hapo.

Mzee Muganyizi alipaki gari lake kwenye viunga vya kampuni hiyo, akashika na kuelekea mapokezini. Alikaribishwa na wahudumu wa kampuni ile, na yeye bila kupoteza muda, akajieleza nini kilikuwa kimetokea na kwamba alitaka

wafanye mpango wa kumrejeshea fedha zake. Mhudumu aliomba kuona vithibitisho vya kuchukua mkopo kwenye kampuni yao. Binti yule mwenye asili ya kiarabu au kiajemi hivi, alichukua mkataba ule na kuutazama vizuri halafu akamuuliza mzee Muganyizi kama hakuwa amesahau makubaliano waliyowekeana na kampuni. Muganyizi alimweleza kuwa hajasahau kwa sababu alikopa Tsh million kumi na walikubaliana angelipa tsh million 11 ikiwa ni pamoja na riba waliyomweleza kuwa ni asilimia kumi tu. Binti yule alimrudishia ile nakala yake ya mkataba na kumwambia asome upya tena kwa sababu yeye hakuona tofauti

ya kilichokatwa na kile ambacho walikubaliana kwenye mkataba ule. Muganyizi aliupokea mkataba na kuuchunguza tena.

Hakuamini!!

Alivuta miwani yake toka kwenye mfuko wa koti na kuivaa, aliinamia karatasi na kusoma tarakimu zilizoandikwa 100,000,000/=. Nguvu zilimwishia, mapigo yake ya moyo hayakueleweka sasa, aliweza kuyasikia yanavyodunda na kuhisi jasho likijaa viganjani mwake. Kama vile kipofu, mzee alipapasa kutafuta kiti, alipofanikiwa kukishika alikaa chini, taratibu lakini kwa yakini, sauti zote ziliaanza kufifia na kubaki kimya, akawa kama yupo kwenye chumba

cha ajabu kisicho na uhai. Kwa muda, akili yake ilikuwa kama imepigwa ganzi. Alitulia kimya, kilichosikika ni mapigo yake ya moyo tu! Nayo yalimfanyia kusudi kwa kule kudunda kwake kulikosikika kwa sauti kubwa ungedhani ni mdundo wa dufu.

Alipofanikiwa kupata nguvu kidogo na kutuliza moyo, Muganyizi alinyanyuka taratibu huku akiyumba yumba, alisimama kidogo, miguu ikapata stamina tena akaendelea na safari yake kuondoka kutoka kwenye viwanja vya kampuni ile. Alilifikia gari lake na kuliwasha na safari ikaanza. Alipokanyaga break, alikuwa anatazamana na bar moja hivi nje kidogo ya mji. Hakuwa mlevi,

alikunywa pombe kali mara chache sana kwa sababu alizodai ni za kitabibu akiwa nyumbani, tena kidogo Sana kwa kipimo maalum. Lakini leo hii, baada ya yale yaliyommaliza nguvu hapo awali, alihisi eneo lile lingeweza kumpa faraja na kumuondolea lindi la mawazo aliyokuwa anawaza bila kuelewa kitu kwa siku hiyo.

Aliingia kaunta, akaagiza pombe kali na kujitafutia kona ya ufichoni na kuanza kuzinywa. Kadri alivyozidi kuzibugia ndivyo lile tukio la jana benki na la leo kwenye kampuni yalivyozidi kumpa maswali kuliko liwazo, alibaini pombe zilikuwa hazimsaidii, alinyanyuka huku akiyumbayumba, akamwita

mhudumu na kulipa bili yake kisha akatoka hapo bar.

Ingawa alikuwa kalewa, bado alikuwa na uwezo wa kuliendesha gari lake. Aliendesha kwa mwendo wa kawaida kuelekea nyumbani kwake. Alipofika kwenye junction ya kuelekea kwenye barabara ya mtaa unaoelekea yaliko makazi yake, aliishuhudia lorry kubwa aina ya scania ikimfuata upande aliko kwa spidi kali sana. Ni kama ulevi ulimtoka ghafla, kitendo kile kikayaokoa maisha yake ambayo yangepotea kwa ajali ya uso kwa uso na scania, gari lake aina ya Noah liligongwa upande wa nyuma na kusukumizwa kwenye mtaro pembezoni mwa barabara. Alichomoka kwenye usukani na

kufanikiwa kutoka ndani ya gari bila kuumia zaidi ya kupata mshituko kwenye mguu wake ambao ulipata kupata kilema cha kudumu kwenye ile ajali iliyompokonya mke wake kipenzi.

Walioshuhudia ile ajali walikiri ulikuwa ni muujiza kwa mzee Muganyizi kutoka akiwa mzima, na kudai dereva wa scania alidhamiria kummaliza yule mzee.

Alipopata fahamu zake vema, Muganyizi alishindwa kuamini kuwa ile ilikuwa ni ajali ya kawaida. Kwa macho yake alimshuhudia dereva wa scania akimfuata kwa lengo la kumgonga. Mambo yaliyokuwa yanamtokea sasa yalimpa hofu kuu,

alijaribu kujituliza kwa kujisemea 'ni mshituko tu, nitakuwa sawa!' Lakini hakupata picha, huenda ajali hutokea namna hii!! Alijiuliza lakini wala hakupata jibu.

Traffic walipowasili walifanya ukaguzi na kuandika faini kwa mzee Muganyizi, kwa madai kuwa alikuwa anaendesha akiwa amelewa na ndio sababu ya ajali. Baada ya kumalizana na matrafic , Muganyizi alifanya utaratibu wa kulitoa gari mtaroni likapelekwa gereji kwa matengenezo! Aliliacha huko na kuamua kuchukua taxi kuelekea nyumbani, alihitaji kupumzika. Aliposhuka kwenye taxi ilimbidi kuvuka barabara kuelekea mtaa wa pili yalipokuwa makazi yake. Alitazama huku na kule barabara

ilikuwa nyeupe isipokuwa pikipiki kubwa aina ya Honda iliyokuwa imepaki pembeni mwa barabara hatua chache tu. Aliingia barabarani, alipofika kati, alitahamaki kuliona lile Honda likiwa limewasha taa likija spidi huku dereva wake akionekana amedhamiria kumugonga, ile kutahamaki, alijikuta mtaroni, mguu wake mbovu ulikuwa unavuja damu gotini, akashukuru Mungu kwa mara ya pili aliokoka ajali iliyolenga kumdhulumu maisha yake. Piki piki lile sasa likiwa limetokomea kizani kwa muda mfupi tu!

Sasa hofu yake ilizidi maradufu, hofu hiyo ikamtuma kuchukua tahadhari, alikumbuka, alipata kuandika namba za simu za kijana mmoja wakili

kwenye kongamano la katiba pale Nkurumah Hall – University of Dar es salaam, jina lake Kajumulo.

Alimpigia simu, akajitambulisha na kumjulisha mazingira aliyokuwa nayo na hofu iliyompata kutokana na ajali hizo mbili na kuhitaji msaada wa kisheria hasa kutokana na utapeli ule aliokuwa amefanyiwa na kampuni ile ya mikopo. Alimaliza mazungumzo huku akimpa mawasiliano na anuani ya makazi yake.

Haikumchukua muda kufika kwake ingawa maumivu ya mguu sasa yalikuwa makali mno. Aliingia getini kwake akiwa Hana hamu kwa madhila aliyokumbana nayo siku hii. Siku ilimchachukia vibaya!

Akadhamiria akiingia ndani hatoki tena hadi kesho, lakini loh! Ile kuvuka kizingiti cha geti mzee akajikuta ana kwa ana na mdomo wa bastola, akahamaki! Kijana mnene, mwenye madevu na masharubu, aliyevalia miwani mikubwa iliyofunika macho yake hadi kwenye uso huku kichwani akiwa na mzula mwekundu alikuwa nyuma ya bastola ile! Moyo ulimlipuka pah! Alipojaribu kumkazia macho, Muganyizi alidondoka chini baada ya kupokea kibao kizito kutoka kwa jambazi Yule, alipojaribu kuinua kichwa chake, Alikutana na macho makavu ya jambazi, yamewiva na kukolea wekundu Kama vile damu zimevilia machoni mwa kijana huyo.

‘Mkataba, nataka mkataba wa mkopo, haraka’ Jambazi aliongea, sauti nzito yenye mikwaruzo, na harufu nzito ya sigara, ugoro au bangi ikamvamia kiasi cha kumfanya Muganyizi akohoe.

Jambazi Yule alidhamiria kukipata alichofuata na si vinginevyo. Sauti yake, mwonekano wake vyote vilidhihirisha hilo!

Kwa hofu na woga, Muganyizi alijibu;

‘Kwenye mkoba kijana wangu, upo humu kwenye mkoba, tafadhali nihurumie kijana, shida zangu zitaniua muda si mrefu, usichafue mikono yako kwa damu yangu nakuomba’ alikuwa anatetemeka.

Jambazi lile lilichomoa makaratasi kwenye mkoba, jina la kampuni ile lilisomeka vema kabisa kwenye makaratasi yale, jambazi kwa furaha likamtazama Muganyizi kwa tabasamu halafu likamuonesha ishara ya kuchinja shingo. Kutahamaki, Muganyizi alidondoka chini mithili ya gogo huku damu zikifoka kifuani mwake!

# 3

Muganyizi alifumba macho yake na kujaribu kusali sala yake ya mwisho. Tayari alihisi malaika mtoa uhai amemtembelea. Damu iliyokuwa inafoka kifuani kwake sasa ilimwelemea  kwa uzito. Akili zake zikamshawishi kufumbua macho ili ashuhudie dakika zake za mwisho, walau aende na picha ya tukio la kufa kwake. La haula! Shabaash! Sasa alibaini chanzo cha uzito ule! Yule jambazi alikuwa kamlalia kifuani mithili ya gogo, kimya kimya akigugumia kwa maumivu na damu zikichuruzika midomoni mwake. Hapo akabaini damu zile hazikuwa zake bali za jambazi yule aliyekuwa kadhamiria kumuua! Hakuelewa

kilichotokea, kumbukumbu zake zilionesha kwamba, kabla ya kuanguka, alishuhudia jambazi lile likinyoosha mkono uliokuwa na bastola kifuani kwake!

Alijaribu kunyanyuka lakini mguu wake haukumruhusu. Katika jitihada hizo, Muganyizi alijikuta akiupokea mkono wa kijana mmoja ambaye alionekana kumsaidia. Hatimaye alimudu kusimama, alipomtazama vizuri kijana huyo, Muganyizi aliishiwa nguvu kabisa! Kama ni balaa, hili lilikuwa ni babalao! Ni kama aliruka majivu na kukanyaga moto. Alimtambua vema, angewezaje kumsahau? Alikuwa kaongezeka uzito, hata ngozi ya uso wake ilikuwa imenawiri vema na kuweka

mnururisho angavu. Bila shaka maisha yalikuwa yamemnyookea kijana huyu! Alijivuta taratibu, akitamani angerudi enzi zake alipokuwa angali kijana mdogo, enzi zile alizomudu kukimbia kila asubuhi kwenda shuleni, peku bila viatu kwa umbali wa maili nane hivi! Lakini sasa hakuwa na ujanja, miguu yake mwenyewe ilikuwa imemchoka, na hata alipoiamrisha, haikumtii tena! Aliilaani kimoyomoyo!

Kijana yule alimsogelea na kumshika bega, Muganyizi mkojo ukamtoka wala asijue, huku ukelele wake wa kuomba msaada, ukiishia kusikika ubongoni mwake, usisikike hata na sikio lake mwenyewe.

‘Pole mzee wangu,’ Yule kijana alitamka. Muganyizi akaona maajabu, hiyo pole alikuwa anapewa yeye au Kuna mtu alikuwa anapita!? Alibaki anamtazama kijana yule asijue nini cha kujibu

‘Sina nia mbaya na wewe, najua unahofia kwa vile ni mimi niliyekusainisha mkataba ambao sasa umekusababishia yote haya’ kijana aliendelea kujieleza. Kidogo mzee huyo ajibu kwa hamaniko, "Ndiyo, ni wewe, ni wewe uliyeniingiza mkenge, Bata mzinga mkubwa wewe", lakini hakuwa hata na ujasiri huo. Alisalia kimya kama zoba.

Muganyizi alibaki kaduwaa asiye na uhakika na hisia zake kwa wakati ule!

‘Mengi yametokea na kwa kweli kilichofanyika dhidi yako nilikuja kugundua baadae na nilipojaribu kuhoji walinigeuka……’ hakumaliza sentensi yake, machozi yalianza kumtiririka kijana huyo, huku akiongea kwa kwikwi akatamka;

‘…. Siamini kama baba yangu amekufa kwa kukosa fedha ya upasuaji wa tezi dume, yote hayo kwa sababu kampuni ilinifilisi kwa madai eti niliwaibia’. Kijana alijifuta machozi na kumalizia;

‘…..mimi pia ni mhanga wa ile kampuni mzee wangu, baba yangu amekufa kwa sababu yao’

Muganyizi sasa alivuta makini yake na kujikuta akimuonea huruma kijana

yule. Huruma ile ikamfanya amkumbuke kijana wake Muta, mwanae kipenzi ambae sasa alikuwa jela, jela kwa sababu hakuwa na pesa ya kumweka dhamana! Machozi yakamtoka mzee wa watu!

‘Hawa watu ni lazima warejeshe fedha zako mzee, nipo tayari kusaidiana na wewe kuhakikisha haki inatendeka na matapeli hawa wanawajibishwa, lakini sasa hapa kuna kazi ya kufanya mzee wangu’ kijana alimaliza kuzungumza huku akijitambulisha kwa jina moja la Aidani.

‘Tunahitaji kuwataarifu polisi kuhusu huu mwili’ Muganyizi sasa alimudu kutamka.

'Ndio mzee, hebu ngoja nikachukue vocha hapo gengeni, simu yangu haina salio la kutosha' Aidan aliongea huku akiashiria kutoka. Muganyizi akakumbuka alikuwa na kifurushi chake cha wiki ambacho alikuwa bado kukimaliza.

'Unaweza kutumia yangu kijana' alitamka huku akimkabidhi Aidan simu yake.

Aidani alichukua simu ya mzee Muganyizi na  kuanza kupiga huku akimkabidhi bastola yake mzee Muganyizi  ambaye aliipokea kwa hofu, akishindwa kusema hapana kwa gagaziko lililompata. Yule kijana akatoka nje ya geti huku akizungumza

kwa msisitizo na huyo aliyempigia simu.

Haikuchukua muda mrefu, kitu kama dakika tano hivi, Muganyizi alisikia ving'ora vya gari za polisi nje ya geti lake. Aligeuka amuone Aidan lakini kijana huyo hakuonekana. Hiyo haikumpa wasiwasi, huenda alikuwa nje kuwapokea polisi! Alihitimisha hivyo. Akajikongoja taratibu kuelekea getini ili kuungana na Aidani kuwapokea polisi, oh daah!! hakuamini macho yake. Polisi wote sita walikuwa wamenyoosha silaha zao dhidi yake alipotokeza getini tu. Hali hiyo kidogo ikamchanganya! Vipi tena polisi wamuone adui? Moyoni alijifariji kwamba ile ilikuwa ni kuchukua tahadhari. Faraja hiyo

ikayeyuka pale alipomsikia afisa mmoja akiwasiliana na mkuu wake, juu ya kumpata muuaji alipojaribu kutoroka, na kudai mwonekano wake ulikuwa sawa kabisa na maelezo ya raia mwema aliyetoa taarifa polisi, tena kuongezea kuwa muuaji alikuwa na bastola mkononi. Kusikia kauli hiyo, kukamnyong'onyeza Mzee Muganyizi.

Muganyizi akageuka huku na kule ili kumuona Aidan ambaye angesaidia kunyoosha maelezo, Aidan hakuonekana! Mara akasikia sauti ya kikamanda kutokea kwenye kipaza sauti kwenye moja ya gari la polisi ikimtaka aweke silaha chini na kujisalimisha kwa hiari kwa Jeshi la polisi.

***

Muganyizi alipiga magoti akairusha bastola mbali kuwaelekea polisi na kunyanyua mikono yake juu ishara ya kutii amri bila shurti. Askari mmoja, bila shaka mkubwa miongoni mwao kwa mwili, sio cheo, kwa tahadhari sana akamsogelea na kumkagua kama alikuwa na silaha nyingine zaidi au la! Zoezi hilo lilipomalizika, Muganyizi aliwekwa pingu na kwa uangalizi wa hali ya juu akatupwa kwenye land Rover la polisi ambapo alijibamiza kwenye chuma cha ukingo wa bodi la gari hilo. Wakati anajaribu kujiweka sawa alishuhudia mwili wa marehemu jambazi aliyeuwawa na Aidan ukidondoka juu yake mithili ya gunia la mahindi. Gari liliondolewa

kwa kasi kuelekea kituo cha polisi. Bila kujitambua, Muganyizi alijikuta kazama kwenye usingizi mzito. Alipokuja kushituka, Muganyizi alijikuta hospitalini, akihudumiwa na nesi, pembeni yake, binti yake Koku akiwa mwenye majonzi tele akiwa anamtazama kwa huruma. Kwa mbali aliweza kumuona askari mwenye silaha akiwaangalia kwa udadisi na tahadhari.

'Baba' Koku alitamka machozi yakicheza chess machoni huku akijitahidi yasidondoke chini.

'Pole baba yangu' chozi like halikuhimili kusalia jichoni, likamdondoka Koku. Muganyizi akajaribu azungumze lakini

akashindwa. Ulimi wake ulikuwa mzito, hakuweza kutamka chochote. Chozi likamtoka. Koku akamkumbatia na kumpa faraja. Kumbato lake likampa tumaini. Kwa mara nyingine tena akajaribu atamke neno, lakini maumivu aliyoyapata hayakuwa na mfano. Sasa aligundua, kwamba taya yake ya kulia haikuwa sawa. Nesi akamweleza kutulia na kutojaribu kuzungumza kwa muda ule kwa sababu taya yake ndo ilikuwa imehudumiwa muda si mrefu.

Katika harakati zile za mshikemshike na polisi, alipojibamiza ubavuni mwa gari, taya yake ilisogea kidogo na kufuatia tukio lile alizima na hio ndo ikawa sababu iliyompelekea kuwepo pale hospitali.

Alipomudu kujongea pale kitandani, Muganyizi alitoa ishara ya kuhitaji kalamu na karatasi. Kwa msaada wa nesi kalamu na karatasi vililetwa na yeye akamudu kuandika maneno yaliyosomeka;

‘Wakili Kajumulo, 071411**08’

Alishusha kalamu na kutuliza kichwa kwenye kitanda, akauruhusu usingizi umvae.

***

‘Wafungwa waua na kuwapokonya silaha polisi magereza, ni gereza la Ukonga’ liliandika gazeti la kisima cha habari.

‘Wanatafutwa kwa mauaji ya polisi magereza’ likahanikiza gazeti la

'matukio' likiwa limedamshi na sura za wafungwa kadhaa na miili ya marehemu askari magereza!

Hivyo vilikuwa ni vichwa vya baadhi ya magazeti vikiwa na picha za baadhi ya watuhumiwa hao. Kwenye mitandao ya kijamii hiyo ndo ilikuwa habari ya siku. Mijadala yote ikilenga tukio kubwa na la kutisha lililokuwa limefanywa na wafungwa dhidi ya polisi magereza.

Koku akiwa pale hospitalini, akifuatilia maendeleo ya baba yake ambaye sasa alikuwa ni mtuhumiwa wa mauaji, alijikuta anadondoka chini na kuzimia.

Habari aliyokuwa amesoma kwenye mtandao kupitia simu janja yake

ilikuwa nzito kupokelewa na moyo wake mwepesi. Miongoni mwa watuhumiwa wale wa mauaji ya polisi alikuwemo Muta kwa mujibu wa habari ile iliyopambwa kwa sura ya mdogo wake Muta kwenye ukurasa wa kwanza tu wa gazeti la mtandaoni. Habari hiyo ikamfadhaisha na kumshitua moyo. Akazimia. Manesi wakamwahisha wodi ya Wanawake na kumpa huduma ya kwanza.

Alipozinduka, alikuwa ametundikwa drip ya maji na kulazwa kwenye kitanda wodi ya wanawake pale hospitalini.

Tukio hilo la kutisha la mauaji ya polisi lilipelekea kuongezwa ulinzi zaidi kwa Muganyizi, huku magazeti

ya udaku yakiunganisha habari ya vifo vya Byarugaba na Rutashobya, tukio la  Muta kuua na kutoroka gerezani na hili la kukamatwa kwa mzee Muganyizi kwa tuhuma za mauaji ya mtu ambaye jina lake halikujulikana haraka na hivyo kuipaka vibaya matope familia ya Mzee Muganyizi.

Habari hizi zikaenea kwa haraka mithili ya mlipuko wa covid 19 na kusambaa kwa kasi na kujizolea umaarufu ulimwenguni kote.

# 4

Miezi miwili ilikuwa imekatika sasa tangu alipohukumiwa kifungo jela kwa kosa la ujambazi na mauaji, kikiwa ni kifungo chake cha mara ya pili baada ya kifungo cha awali ambapo alituhumiwa kutapeli pesa kwenye kampuni moja ya usambazaji wa filamu za kibongo pesa nyingi. Kwa sehemu sasa alikuwa ameyazoea maisha ya jela. Safari hii, Muta alimudu kutazama upande wa pili wa maisha kwa mtazamo tofauti na ule wa awali. Mtazamo uliomuonesha kuwa zaidi ya pesa na matumizi yake, maisha yalikuwa na maana pana zaidi ambayo huenda hakuna binadamu aliyemudu kutoa tafsiri yake toshelevu.

Akiwa kwenye kona yake aliyozoea kulala mle gerezani, eneo chafu kabisa kwa mtu wa haiba yake kuishi, alikuwa kazama kwenye dimbwi la tafakuri nzito, akitafakari hali yake ile ambayo hakuelewa nini hatima yake. Zaidi alimlaumu sana baba yake kwa kushindwa kumtoa katika  hali ile ya mateso, wakati alijua fika kuwa mzee wake alikuwa anachukua mafao yake mwaka huo. Alijitazama na kuona alivyokuwa amedhoofika. Siku za mwanzoni, alishindwa kula kabisa chakula cha jela, ugali uliopikwa kwa pumba za mahindi na hata wakati mwingine pumba za ngano, ndondo zilizosheheni wadudu wadogo weupe na weusi, mbaya zaidi ndondo zenyewe zikihesabika ukiacha bahari

ya maji moto yaliyochemshwa na kutiwa chumvi eti ndio mchuzi. Haikuwa rahisi kuzoea. Kwa bahati mbaya sana pia, hakuna aliyeonesha kujali. Alipobaini hakuna anayejali na kwamba hata kama angelikufa kusingekuwa na tofauti, aliazimia kuikubali hali ile. Alianza kwa kujilazimisha kula na hatimaye ratiba ya chakula cha jela ikamkaa vema kichwani. Maisha yakasonga. Afya yake ikarejea. Akaanza na mazoezi ya mwili, mwili ukakubali. Akapata heshima na kujipatia ukubwa gerezani. Mwenyewe akijiita mtemi.

Leo hii akiwa kwenye kona yake pendwa, alikuwa peke yake, utemi wake ukiwa umevuliwa rasmi, wapambe wake wote akiwa

amewapoteza baada ya kutokea mbabe zaidi yake pale gerezani.

Gerezani alikuwa kaingia jabali la mtu, hakujulikana jina, ingawa wafungwa wenzie sasa walimbatiza jina 'Nondo'. Nondo alikuwa amehukumiwa jela kwa kosa la kupora kwa kutumia silaha. Tukio ambalo lilihusisha mauaji ya kutisha ya tajiri mmoja maarufu sana kwa jina la Mr. Masebo (Pedezyee Sebo), mfanyabiashara wa vinyago jijini Dar es salaam na mmiliki wa club za usiku mbalimbali jijini humo. Mr. Masebo kwa upande wa pili alikuwa ni mtu hatari sana ikisemekana kwamba alikuwa miongoni mwa waagizaji nguli wa madawa ya kulevya nchini, akiwatumia zaidi wasanii wa bongo

muvi, wanamitindo, na wanamuziki kama punda wa kufanikisha biashara zake hizo, wakibebeshwa madawa hayo toka nchi moja kwenda nchi kusudiwa. Pia, ilijulikana kuwa alikuwa na hisa nyingi kwenye makampuni mbalimbali ya kifedha nchini. Taasisi za ukopeshaji fedha kwa riba.

Kwa taarifa za uhakika kutoka kwa waliohudhuria hukumu ya Nondo pale mahakamani, zilidai kwamba Nondo aligundulika kuhuska na mauaji ya Mr. Masebo kutokana na taswira yake kunaswa kwenye camera za CCTV zilizokua zimetandazwa kuzunguka mjengo wake wa kisasa uliokuwa nje kidogo ya jiji la Dar es salaam maeneo ya Mkuranga mkoani

Pwani. Jengo hilo matata la Mr. Masebo lilikuwa na walinzi wenye mafunzo maalum lakini Nondo alifanikiwa kupenya na kuinyofoa roho ya Masebo na kutokomea zake huku akiwaacha walinzi wale katika ulemavu wa kudumu. Tukio hilo likamfanya Nondo kuwa miongoni mwa majambazi hatari waliokuwa wanatafutwa na mkono wa sheria.

Kukamatwa kwake ilisemekana kulikuwa kwa kizembe sana kwa mtu wa kaliba yake. Alikamatwa katika club mojawapo ya Mr. Masebo akiwa anakula raha na watoto wawili wa kike kutoka arabuni. Mmoja kushoto kwake na mwingine kulia kwake. Wanawake warembo na wenye kujua

kutumia miili na maumbo yao Kama kitega uchumi.

Wakati polisi walipomfikia, Nondo hakuonesha jitihada zozote za kujitetea au kukimbia. Alitii amri bila shurti. Ima alishindwa ujanja kutokana na eneo alilokuwa au hakujua kilichokuwa kinamkabili. Lakini hata kama alihusika, basi huyu hakuwa yule Nondo hatari kama alivyotambulika kote jijini. Huyu huenda kaponzwa na ufanano wake na Nondo. Polisi wale wakahisi hivyo, maana Jamaa huyu alikuwa kondoo. Alichojua labda ni Wanawake tu. Polisi hawa walielekea kuamini hivyo.

Nondo aliswekwa rumande kungojea kupelekwa kwa shauri lake

mahakamani. Kwa vile kesi yake Ilikuwa yenye kuvuta makini za raia na wafuatiliaji wa mambo, shauri lake lilienda mahakamani mapema, huku upelelezi ukishika hatamu kwa mwendo kasi.

Kesi yake haikuchukua muda, ilimalizika haraka kwani Nondo alikiri makosa aliyokuwa amesomewa. Alipoulizwa kama alimuua Mr. Masebo, Nondo alijibu kwa kujiamini kabisa mbele ya hakimu kwamba ni kweli alihusika na kumuua Mr. Masebo na kwamba angepata habari kuwa hakufa basi wasingemkamata kwa sababu angehakikisha Masebo anakufa kwanza kabla ya yeye kuonekana mbele za mtukufu hakimu. Alidai kwamba kwa vile serikali ilijua

maovu ya Mr. Masebo lakini ikaamua kufumbia macho, basi watu wa aina yake walihitaji kuzaliwa zaidi ili kudhibiti kuangamia kwa wengi kulikotokana na matajiri wachache sampuli ya Mr. Masebo kujitajirisha huku wakitumia binadamu wenzao mithili ya mipira ya kuvaa uumeni wakati wa ngono na kutupiliwa mbali baada ya tendo hilo.

Kwa kuzingatia ushahidi wa camera na tamko lake mwenyewe, hakimu alimuhukumu Nondo kwenda jela kwa miaka 30 kama onyo kali kwa wengine wenye tabia kama yake.

Nondo akakutana na Muta kwenye gereza la Ukonga na huzuni ya Muta ikawadia. Nondo alivyoingia gerezani

ikawa ni mwisho wa utemi na ubabe wa Muta gerezani.

Alipoingia jela, Nondo akakutana na sifa na hofu iliyotawala mle gerezani kutoka kwa mtu aliyejulikana kwa jina la Muta. Basi yeye Nondo akacheeeka kweli. Cheko la dharau. Hakutaka kuamini kuwa kuna mtu mwenye sifa zile mle gerezani.  Naam, labda kwa sababu aliingia gerezani kwa kupenda na kwa lengo maalum. Au labda yeye alikuwa na sifa zaidi ya hizo alizoaminishwa kuwa ni za kipekee. Kabla ya kuoneshwa malazi yake yatakapokuwa, wapambe wa Muta walimfuata na kumpleka mputa mputa kwa bosi wao! Alipofikishwa mbele ya mtemi, aliamriwa kupiga magoti na kutoa heshima kwa mtemi

wao. Ndio, Muta sasa alikuwa ni amiri jeshi kwenye jeshi aliloanzisha gerezani. Alikuwa ni mtawala mwenye heshima kubwa. Heshima iliyotokana na kumpindua mtabe aliyekuwepo kabla hajaingia gerezani. Mfungwa aliyejulikana kwa jina Pandu. Heshima hii, Muta aliipata baada ya kuingia kwenye pambano na Pandu na kufanikiwa kumchakaza vibaya kwa kipigo. Pandu akapigwa marufuku kushiriki kwa namna yoyote ile kwenye harakati ambazo zingeonesha anataka kupata kiti chake. Muta akatangaza serikali ya kiimla yeye mwenyewe akiwa ndio dikteta kwenye serikali hiyo.

Katika kujihakikishia kuwa anadumisha utawala wake gerezani,

Muta akatengeneza propaganda nyingi na kuzieneza gerezani. Raia wake wakaziamini, sifa zake zikawa kemkem. Wengi wakiamini ni kweli Muta alikuwa na uwezo wa juu zaidi wa kichawi. Kwamba alikuwa na nguvu ambazo hakuna mchawi angeweza kufikia. Akawajaza watu wake hofu , akaanzisha mfumo wa kodi kwa kila kichwa gerezani. Kodi hiyo ilikusanywa kila mfungwa alipotembelewa. Chochote alicholetewa, asilimia 40 ilimegwa kupelekwa kwa mtemi. Wafungwa wapya walijazwa simulizi za kutisha za Mtemi Muta, simulizi ambazo wala hazikuwahi kutokea. Muta kwa sehemu kubwa akaishi jela kama mtawala na maisha yake yakiwa sawa

na raia wa kawaida nje ya gereza isipokuwa Uhuru wa kuzurura..

Nondo alipofikishwa mbele ya mtemi na kulazimishwa kupiga magoti, alikataa kutii amri. Kitendo hicho kikamkasirisha sana mtemi. Muta akafanya jitihada ya kuamka ili kumuadabisha mfungwa huyu mgeni. Hata hivyo askari wake mtiifu akamuomba yeye ndo amuoneshe mshenzi yule ambaye hakutaka kufuata sheria za serikali ya Muta, nini maana ya kutii amri. Ngeumkeni akarusha ngumi moja yenye uzito wa kilo tano hivi na point kadhaa. Ngumi hii ililenga kuutawanya kabisa uso wa Nondo, lakini kwa ustadi wa hali ya juu, Nondo akaepa, na kumshindilia Ngeumkeni konde moja lililompata

barabara panapo mbavu zake, Ngeumkeni akadondoka chini mithili ya gunia la viazi na kulamba vumbi miguuni pa Nondo. Kuona vile askari wengine wa Muta wakajazwa upepo wa hasira, wakamvamia Nondo kwa pamoja. Tayari raia wa gereza la ukonga wakawa wamekusanyika kushuhudia pambano hilo kali dhidi ya serikali ya Muta na muasi mmoja aliyejiita Nondo. Kwa mpambano uliokuwa unaendelea, ni dhahiri muasi huyu alikuwa amejipatia wafuasi wa kutosha. Zilisikika kelele nyingi za kumshangilia kutokana na uwezo aliouonesha. Hofu ikamvaa Muta, hasira zikamjaa hadi pomoni, alikuwa anadhalilishwa, na hakujua angekuwa nani bila utemi wake mle

gerezani. Asingeshindwa kizembe, angewezaje kuikabili aibu, na si wote walimuogopa kwa zile sifa zake za kichawi? Na ule ustadi wa kumng'oa Pandu?

Wapambe wa Muta walivyoshuhudia ile hasira yake, wakajua Nondo atapoteza maisha yake. Wakajaribu kumsihi Nondo aombe msamaha kama anapenda uhai wake. Wakamhakikishia kwamba hakuna mtu angeweza kufanya kitendo kile alichofanya na abaki salama katika utawala wa Muta. Wengi waliamini kilichokuwa kinafuata ni mazishi kwa Nondo. Nondo kusikia hivyo ndo kwanza akacheeka sana tena kwa dharau iliyomchanganya zaidi Muta.

Muta akaendelea kumkazia macho Nondo moyoni akitamani ushawishi wa propaganda zake uliokuwa unafanywa na wafuasi wake watiifu dhidi ya Nondo utazaa matunda. Ah! wapi? Nondo ndo kwanza alizidi kuonesha unondo wake. Muta akafanikiwa kutamka kwa sauti tetemeshi,

'Wewe ni nani unayediriki kujeruhi askari wangu, unadiriki kusimama mbele zangu kwa kiburi na majivuno! Haa! Hunijui kwa kweli! Usipojirudi nakurudi, iwe mfano kwa wengine wanaodhani wanaweza kuleta ujinga kama huu kwenye utawala wangu, mimi ndio Muta, …..' hakufanikiwa kumaliza maelezo yake kwa hadhira, Kwa dharau kubwa, Nondo

alimgeuzia Muta kisogo na kuwakabili wale raia wa gereza ambao walilipuka kwa kelele za kushangilia. Nondo aliwatazama washangiliaji wale kwa jicho la kujionesha yeye ni bingwa halafu akawanyamazisha kwa ishara ya kuweka kidole cha pili baada ya gumba lake mdomoni na kutoa sauti ya ‘sh-sh-sh’. Gereza na wafungwa wale kwa umoja wao wakatekwa na ukimya wa ghafula, nadhani kwa shauku ya kusikia muasi alitaka kusema nini.

“Ati naulizwa mimi ni nani? Nitawaambia, mimi naitwa Buda aka Nondo, muuaji ambaye ametukuka, muuaji wa mafisadi na watu wenye kuonea wanyonge. Naam, naitwa

Nondo. Kama wewe ni fisadi, basi time (muda) yako imefika upate hukumu unayostahili. Wewe ni adui wa Nondo na lazima utashughulikiwa vilivyo!" Nondo akamaliza, lakini ile ageuke kumtazama Muta, Muta akamvaa Nondo mzimamzima na kumwangusha chini, akawa amekaa juu yake, lakini katika hali ambayo watu hawakutarajia, walimshuhudia Muta akipaa juu na kisha kutua hatua chache kidogo mbele ya Nondo kwa kishindo kikuu! Nondo akamfuata Muta na kisha akamnyanyua juu mithili ya katoto kadogo. Muta akawa amedhilika kupita kawaida.

'Bila shaka huyu naye ni fisadi, kwa sasa nitampa onyo, na nitafanya uchunguzi wangu taratibu,

nitakapobaini ufisadi wake, nitamhukumu sawasawa na sheria zangu dhidi ya mafisadi' gereza likarindima kwa kelele za shangwe, wafungwa wale wakifurahia mapinduzi yaliyokuwa yamefanyika dhidi ya dikteta wao Muta.

*Je huu ndio mwisho wa serikali ya Muta gerezani? Nini hatima ya mzee Muganyizi? Nondo ni nani hasa? Kwa majibu ya maswali hayo na mengineyo, fuatilia mkasa huu wenye kufundisha, kuburudisha na kufurahisha.*

KWA TSH 3000/= TU UTAPATA SIMULIZI HII KWA UKAMILIFU.

TUMA PESA YAKO KWA **M-PESA 0744-50-94-65** AU **HALOPESA 0629-**

**07-77-92**. DAVID NGOCHO SAMSON NDIO MAJINA YA MPOKEAJI.

ASANTE SANA KWA KUUNGA MKONO KAZI ZANGU. UBARIKIWE!